Upumbavu wa Kuamini katika Hekima za Mwanadamu

Na

Ellis P. Forsman

(The Folly Of Trusting In Human Wisdom)

Oktoba 15, 2011

Upumbavu wa Kuamini katika Hekima za Mwanadamu

1 Kor. 1:18-31

Leo hii, tunakumbwa na mambo mengi ambayo watu hawakubaliani nayo…

Maadili yanayohusiana na jema au baya. Maswala ya mafundisho yanayohusiana na kilicho jema na baya.

Haijazoeleka kusikia watu wakikubaliana na "mamlaka" fulani. Wale wanaochukuliwa kuwa ni wataalamu katika eneo la sayansi, filosofia, na dini. Wale wanaoambiana matokeo ya uchunguzi wao, majaribio, au wanaofikiri kwa makini.

Wengi wameweka imani yao kwa "mamlaka" kama hayo. Hasa katika eneo la maadili na ukweli wa kiroho. Je hilo ni jambo la busara kufanya?

Katika fungu letu la somo hili (1 Kor. 1:18-31, mtu Paulo anaonya kuhusiana na upumbavu wa Kuamini katika Hekima zaa Wanadamu." Katika kifungu hiki cha maandiko tunajifunza kwamba…

Mungu ameigeuza hekima ya mwerevu kuwa upumbavu

Kumbuka ujumbe wa msalaba…

Wazo wa mwokozi aliyesulibiwa, akifa kwa ajili ya dhambi ya ulimwengu.

Kwa wale wanaopotea, ni upumbavu.

1 Kor. 1:18, "*Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali sisi tunookolewa ni nguvu ya Mungu.*"

Kwa wale wanao okolewa, ni nguvu ya Mungu.

Upuzi wa ujumbe ni kwa mtindo.

Mungu alisema kwamba ataangamiza hekina ya werevu.

1 Kor. 1:19, "*Kwa kuwa imeandikwa, nitaiharibu hekima yao wenye hekima na akili zao wenye akili.*"

Mungu ameipa upuzi akili ya ulimwengu huu.

1 Kor. 1:20, "*Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu.*"

Kwa nini? Kwa sababu dunia katika hekima yake inamkataa Mungu

1 Kor. 1:21, "*Kwa maana katika hekima ya Mungu dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa.*"

Tunaona hilo katika ibada ya sanamu ya siku za Paulo.

Rom. 1:18-23, "*Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu wapingao kweli kwa uovu. Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele wa Uungu wake; hata wasiwe na udhuru; kwa sababu walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo.*"

Tunaiona leo katika mifumo ya mabadiliko, ubinadamu, na uasherati.

Hivyo, Mungu alichagua kumwokoa mwanadamu kupitia imani katika ujumbe ulioonekana kuwa ni upumbavu.

1 Kor. 1:21, "*Kwa maana katika hekima ya Mungu dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa.*"

Wakati Wayahudi walipokuwa wakitafta ishara, na Wayunani wakatafuta hekima.

1 Kor. 1:22, "*Kwa sababu Wayahudi wanataka ishara, na Wayunani wanatafuta hekima.*"

Lakini kwa wale wanaoitikia wito wa ujumbe wa Kristo aliyesulibishwa, kuna nguvu na hekima!

1 Kor. 1:23-24, "*Bali sisi tunamhubiri Kristo aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi; bali kwao waitwao Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu.*"

Maana upumbavu wa Mungu una hekima kuliko wa mwanadamu, udhaifu wake una nguvu kuliko wa mwanadamu.

1 Kor. 1:25, "*Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu.*"

Hivyo, siyo werevu wengi, wenye uwezo, wenye cheo wanaoitwa.

Korintho hakukua na werevu wengi (kulingana na mwili), wenye uwezo, wema walioitikia wito wa injili.

1 Kor. 1:26, "*Maana ndugu zangu angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa;*"

Hiyo ni kweli hata leo: wale wanaoipokea injili mara nyingi siyo werevu, wenye nguvu, wenye hekima ya mwilini, wenye cheo. Tena huu ni mfumo wa mtindo wa Mungu kuhaibisha hekima zenye ukengeufu na nguvu zao wale wanaomkataa Mungu.

1 Kor. 1:27-28, "*Bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam, vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe viwe vilivyoko.*"

Vinginevyo, wenye hekima na uwezo wangejisifu mbele za Mungu.

1 Kor. 1:29, "*Mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu.*"

Hii inaweza kutufanya tutiliyeshaka chochote kinachoendana na hekima au uwe wa mwanadamu. Mwanadamu katika hekima na nguvu zake hawezi kuanza kujilinganisha na upumbavu na udhaifu wa Mungu! Hivyo…

Tunapaswa kujisifu kwa Bwana , siyo mwanadamu

Kwa maana katika Kristo aliyesulibishwa, mwokozi aliyefufuka…

Kuna hekima inapatikana kwa Mungu.

- 1 Kor. 1:30, "*Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi;*"
- Kol. 2:3, "*Ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika.*"

Kuna haki na utakaso.

- 1 Kor. 1:30, "*Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi;*"
- Fil. 3:9, "*Tena nionekane katika yeye nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani;*
- 1 Kor. 6:11, "*Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Krsito, na katika Roho wa Mungu wetu.*"

Kuna ukombozi toka dhambini.

- 1 Kor. 1:30, "*Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi;*"
- Efe. 1:7, "*Katika yeye huyo kwa damu yake tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi sawasawa na wingi wa neema yake.*"

Hivyo, tunapaswa kujisifu katika Bwana.

Kama ilivyoandikwa katika maandiko.

1 Kor. 1:31, "*Kusudi kama ilivyoandikwa, yeye aonaye fahari, na aone fahari juu ya Bwana.*"

Siyo katika hekima yetu, uwezo, au utajiri.

Yer. 9:23, "*BWANA asema hivi, mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake;*"

Bali katika ufahamu na kumjua Mungu, anayefurahi katika upendo, hukumu, na haki duniani.

Yer. 9:24, "*Bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua ya kuwa mimi ni BWANA, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema BWANA.*"

Paulo anajitoa mwenyewe kama mfano.

Ana sababu nyingi za kujisifu

- Gal. 1:13-14, "*Maana mmesikia habari za mwenendo wangu zamani katika dini ya Kiyahudi, kwamba naliliudhi kanisa la Mungu kupita kiasi, nikaliharibu. Nami naliendelea katika dini ya Kiyahudi kuliko wengi walio hirimu zangu katika kabila yangu, nikajitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zangu.*"
- Fili. 3:4-6, "*Walakini mimi ningeweza kuutumainia mwili. Mtu ye yote akijiona kuwa anayo sababu ya kuutumainia mwili, mimi zaidi. Nalitahiriwa siku ya nane, ni mtu wa taifa la Israeli, wa kabila ya Benyamini, Mwebrania wa Waebrania, kwa habari ya kuishika torati ni Farisayo, kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi kanisa, kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia.*"

Na bado akahesabu mambo hayo kuwa kama mavi, kwa ulinganifu wa kumjua Kristo na wokovu wake.

Fil. 3:7-11, "*Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. Naam, zaidi ya hayo nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo; tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenye ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani; ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake; ili nipate kwa njia yo yote kuifikia kiyama ya wafu.*"

Hivyo, kujisifu kwake ilikuwa katika msalaba wa Kristo.

Gal. 6:14, "*LAkini mimi hasha nisione fahari juu ya kitu cho chote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu.*"

Unajisifu katika nini?

Unaweza kujidhania mwerefu, mwenye nguvu, au una jitosheleza kwa sababu ya utajiri wako. Unaweza kufikiria ni busara wengine wakuongoze katika mambo yahusuyo ukweli na maadili.

Lakini isipokuwa ndiye Bwana anayetuongoza, ni upumbavu!

Hitimisho

Kila wakati ntunasikia na kusoma baadhi ya wataalam au mamlaka wanaotoa mawazo ya walichokisomea, baadhi husimama ambapo wengi huonyesha imani yao, tunafanya vyema kukumbuka:

1 Kor. 1:20, "*...Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu?*"

Ukweli pekee na chanzo cha hekima inatoka kwa Bwana mwenyewe…

- Kol. 2:3, "*Ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika.*"
- Kol. 2:10, "*Na ninhyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa chaa enzi yote na mamlaka.*"

Hivyo Paulo anaonya: Kol. 2:8, "*Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo.*"

Je unapenda kuweka tumaini lako, uhai wako, ulinzi wako wa milele, katika mikono ya mwanadamu? Ni bora kiasi gani kuamini katika maneno na hekima ya Muumba na Mkombozi!